**SHULE ZA UPILI ZA ANESTAR**
**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**
**MUHULA WA KWANZA 2023**
**MUDA: SAA 1 ½**

**Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendekei.
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki,
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwene ni Rafiki,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakizifuata nyago,
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Pindi kinunua kitu, harufahi shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekezezok,
Tamko lake "Subutu!" kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Aliye na taradhani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faradhani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Kwa hakika ni baloaa, kumkirimu mchawi, aliyajaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sodawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaniyo,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho change kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa,
Ama nitimue mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamma, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

(a) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 1)

Binadamu hatosheki; Ana tamaa; tamaa ni hatari

(b) Mtungaji analalamika juu ya nini? (alama 3)

- Mtu aliye na tama huwa hatari kama nyika; unafiki wa mtu asiyeaminika; masengenyo, balaa ya kumkirimu mchawi ni kutupiwa kinyesi.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(c) Hili ni shairi la bahari gani? Toa sababu. (alama 2)

- Shairi hili ni la bahari ya tumbuizo kwa sababu kila mshororo una vipande vitatu, ukwapi, utao na mwandamizi, ambavyo vinatoshana kwa urefu. Kila kimoja kina mizani nane.

(d) Kifafanue kibwagizo cha shairi hili. (alama 3)

- Mtu akiwa mwenye tama, wa kutamani kitu kisichokuwa chake, ni hatari kama nyoka. Mtu kaama huyo anaweza kuua.

(e) Andika ubeti wa tatu na wa nne katika lugha ya nathari: (alama 5)

Pindi ukinunua kitu, shetani harufahi bali hujawa na chukizo.
Mtu akiwa mtukutu atanuna mtimani kwa sababu ya tekelezo lako. Tamko lake huwa, "Subutu?" ili akuondoe tumaini na kuliua wazo ulilokuwa nalo.l
Ni taabu kuishi na mtu aliye na taraghani kwani kazi yake ni kujidai. Atakusema faraghani asivyosema ukiwa naye kuwapendeza maadui zako.
Ni mtu akuchimbaye. Hana faida nyumbani. Mradi usimtumai. Mtu aliye na tamaa, wa kutaka kisicho chake, ni hatari kama nyoka.

(f) Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumika: (alama 2)

(i) zani – kitu kinacholeta hasara au madhara; balaa (baa); janga.

(ii) mipangoyo kwake jaa – mipango yako kwake ni takataka.

(g) Kwa kurejelea mifano kutoka katika shairi, taja na ufafanue mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi. (alama 4)

(I) Takriri – urudiaji wa kituo – mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.
(ii) Tashbiha – ni hatari kama nyoka.
(iii) Tashhisi – bahati inahadaa. Bahati imepewa uwezo wa kudanganya
(iv) Litifati – 'Subutu' kumwacha mtu ajisemee
(v) Inkisari – ukweliwe' badala ya 'ukweli wake', 'iso' badala ya 'kisicho' na kadhalika'
(vi) Kugeuza sarufi: "Ninacho change kilio' badala ya 'Ninacho kilio changu' na kadhalika.
(viii) Nahau: Kinyeshi nimetupiwa.

**<u>SEHEMU B: SARUFI (ALAMA 40)</u>**

(a) Bainisha sauti zenye sifa zifuatazo (alama 2)

(i) Irabu ya mbele, juu tandazwa
|i|
(ii) Kipasuo si ghuna cha kaakaa laini
|k|
(iii) Nazali yam domo
|m|
(iv) Kikwamizo ghuna cha meno na ulimi
|ch|

(b) Bainisha silabi funge katika maneno yafuatayo. (alama 2)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(a) Insha - In - sha

(b) maktaba – mak-ta-ba

(c) Tunga sentensi ya neno moja yenye muundo ufuatao. (alama 3)
(i) Kiwakilishi tegemezi cha nafsi ya tatu wingi
(ii) Kiambishi cha njeo ya wakati ujao
(iii) Yambwa tendewa
(iv) Mzizi
(v) Kauli ya kutendea
(vi) Kiishio

**Watampigia**

(d) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)
(i) Mtopetope **U-I**

(ii) Uga **U-ZI**

(e) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao
N + V + Ts + T + N + T + E (alama 4)
**Mwalimu mfupi alikuwa anafunza wanafunzi wakiwa uwanjani.**

(f) Andika sentensi ifuatayo upya huku ukitumia visawe vya maneno yaliopigiwa mstari. (alama 3)

Baada ya Nyanya kuanguka karibu na njia alitokwa na damu puani.

**Baada ya bibi kuanguka karibu na baraste alitokwa na ngeu puani.**

(g) Kwa kutungia sentensi onyesha matumizi matatu tofauti ya "KI" (alama 3)

**(i) Mfululizo wa vitenzi, mama alikuwa akipika huku akilisha mtoto**
**(ii) Masharti: Ukicheza utaanguka mtihani.**
**(iii) Udogo wa nomino: Kibuzi kile ni cha kizee kile.**
**(iv) Kiambicha cha ngeli (KI-VI): Kijiko kimepotea.**

(h) Andika kitenzi hiki katika wingi hali ya kuamrisha (alama 2)
Toka - **Tokeni**

(i) Akifisha sentensi ifuatayo (alama 2)
mama mama mtoto aliita
**"Mama! Mama!" Mtoto aliita.**

(j) (i) Karimu ni kwa choyo sifu ni kwa kukashifu na haba ni kwa tele (alama 2)

**(ii) Maarufu ni kwa mashuhuri, ukoo ni kwa nasaba/mbari ilhali faida ni kwa chumo** **(alama 2)**

(k) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo jedwali. (alama 4)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Shangazi aliuza gari alilopewa na kaka.

| S | | | |
|---|---|---|---|
| **KN** | **KT** | | |
| **N** | **T** | **KN** | |
| | | **N** | **S** |
| **Shangazi** | **aliuza** | **gari** | **alilopewa na kaka** |

(l) Bainisha virai katika sentensi ifuatayo (alama 3)

Mtoto mchafu sana alipigwa vibaya

K.N K.V K.T

(m) Andika sentensi zifuatazo ukifuata maagizo katika mabano (alama 2)

Baba alimpikia mama uji kwa sufuria.

(Anza kwa kipozi)

**Uji ulipikiwa mama na baba kwa sufuria.**

(n) Eleza maana ya ngeli (alama 1)

**Uanishaji au upangaji wa nomino katika makundi yake.**

**SEHEMU C: FASIHI SIMULIZI: (ALAMA 20)**

Ewe Mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudisha vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Ujitaji wetu ukatutuma
Kuokota vihela ulоturushia
Ukatununua, kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Maina wa Ndumi huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama
Wanyonge tumeamua
Kwingine kujaribu.

**MASWALI:**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(a) Huu ni wimbo wa aina gani? Kwa nini? (alama 2)

- Ni wimbo wa kisiasa. Umetaja kura na ubunge.

(b) Andika mbinu za lugha zilizotumiwa katika utungo huu (alama 4)

- Sitiari – vifaranga ni istiari ya watoto
- Maswali ya balagha – ubeti wa kwanza – siwe uloambia akina mama … njaa isiwaangamize?
- Ubeti wa pili – Siwe ulopita Chumvi na Sukari kuturushia ja samadi?
- Uhitaji wetu ukatutuma …. Kura ukapata?
-Tashbihi – Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
- Tashhisi – Uhitaji wetu ukatutuma (uhitaji umepewa uwezo wa kutuma).
- Usambamba – siwe uloambia akina mama … siwe uliopita …

(c) Ni nani anayezungumza (nafsi neni) katika utungo huu? (alama 2)

Mnyonge/mpigakura mwanamke ndiye anayezungumza.

(d) Fafanua toni ya utungo huu (alama 2)

- Wimbo una toni ya kusuta. Nafsineni/mzungumzaji analalamikia usaliti wa mbunge wao na kumsuta kwa vitendo hasi.

(e) Fafanua umuhimu wa nyimbo za aina hii. (alama 10)

- Kukashifu uongozi dhalimu.
- Kuzindua.
- Kutangaza kaulimbiu za vyama vya upinzani au vyama tawala.
- Kueneza propaganda za kisiasa.
- Kusifu viongozi waadilifu
- Kuimarisha uzalendo miongoni mwa wanajamii
- Kuadilisha.
- Kukuza umoja miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, nyimbo za taifa huhimiza umoja.
- Huonyesha migogoro kati ya watawala na watawaliwa.
- Hutambulisha jamii kwa kuonyesha mfumo wake wa kisiasa.
- Huonyesha matarajio ya watawaliwa kwa viongozi.
- Huonyesha historia ya jamii husika.
- Huburudisha.

**SEHEMU D: CHOZI LA HERI (ALAMA 20)**

"Pole pole vilio hivi vilianza kupungua; njaa na ugonjwa vimefanya kazi!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

Msemaji ni ndugu Kaizari
Anamnenea Dkt. Ridhaa.
Walikuwa kwenye kambi ya wakimbizi kwenye msitu wa mamba.
Ndugu Kaizari alikuwa akimsimulia Dkt Ridhaa hali iliyokuwa baada ya kutawa zwa kwa kiongozi mpya na mapigano kutokea.

(b) Bainisha mbinu zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(i) Tashhisi, njaa na ugonjwa vimefanya kazi
(ii) Nidaa – vimefanya kazi!

(c) Fafanua matatizo yanayowakumba wakimbizi katika kambi za wakimbizi. (alama 12)

- Vifo kutokana wa magonjwa kama vile homa ya matumbo
- Ukosefu wa chakula kunawapelekea wakimbizi kula mizizi mwitu.
- Wakimbizi wanakosa maji safi ya kunywa.
- Ukosefu wa misala unasababisha matumizi ya sandarusi hali inayosababisha ugonjwa wa kipindupindu.
- Ukosefu wa malazi na mavazi; mfano Subira na wanawe, Lime na Mwanaheri wananyeshewa kwa kukosa malazi.
- Ukosefu wa faragha kwa ukosefu wa malazi wanaobahatika kuwa na vibanda ndivyo sebule, chumba cha malazi.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes